









# Uamuzi

-  Ursula Nafula
-  Vusi Malindi
-  Ursula Nafula
-  Kiswahili
-  Level 2




Kijiji changu kilikuwa na matatizo mengi. Tulipanga foleni ndefu tukisubiri kuchota maji kutoka mfereji mmoja.




Tulisubiri kupokea msaada wa chakula.




Tulifunga nyumba zetu mapema  
kwasababu ya wizi.




Watoto wengi waliacha shule.




Wasichana wadogo walifanya kazi kama watumishi kwenye vijiji vingine.



Wavulana wadogo waliranda randa kijijini na wengine walifanya kazi kwenye mashamba ya watu.



Upepo ulipovuma, ulipeperusha karatasi chafu na kuzifikisha mitini na uani.



Watu walikatwa na vipande vya chupa vilivyotupwa ovyo ovyo.




Halafu siku moja, mfereji wa maji ulikauka na mitungi yetu ikawa kawa tupu.



Baba yangu alitembea kutoka nyumba hadi nyumba akiwaomba watu kuhudhuria mkutano wa kijiji.



Watu walikusanyika chini ya mti mkubwa na kusikiliza.




Baba yangu alisimama na kusema,  
“Tunahitaji kusaidiana kutatua  
matatizo yetu.”



Juma, mtoto wa miaka minane aliyekuwa amekaa kwenye tawi la mti, alisema kwa sauti, “Naweza kusaidia na usafi.”



Mwanamke mmoja alisema, “Sisi wanawake tunaweza kuungana na kuotesha chakula.”



Mwanamume mwingine alisimama na kusema, “Wanaume watachimba kisima cha maji.”



Sote tulisema kwa sauti moja,  
“Lazima tubadilishe maisha yetu.”  
Tangu siku hiyo, tulifanya kazi  
pamoja kutatua shida zetu.



# Storybooks Canada

[storybookscanada.ca](http://storybookscanada.ca)

## Uamuzi

Written by: Ursula Nafula

Illustrated by: Vusi Malindi

Translated by: Ursula Nafula

This story originates from the African Storybook ([africanstorybook.org](http://africanstorybook.org)) and is brought to you by [Storybooks Canada](http://Storybooks Canada) in an effort to provide children's stories in Canada's many languages.



This work is licensed under a Creative Commons  
[Attribution 4.0 International License](https://creativecommons.org/licenses/by/4.0/).